

MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA AGOSTI 2017 NA MWELEKEO WA SEPTEMBER, 2017

Dondoo za Septemba 2017

Taarifa hii inatoa muhtasari wa hali ya viashiria vya hali ya hewa na mwenendo wa mvua katika mwezi uliopita na mwelekeo wa viashiria, hali ya joto na mvua kwa mwezi Septemba 2017 nchini.

- a) Vipindi kadhaa vya upepo mkali vinatarajiwa kuendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo ukanda wa pwani ya Kusini katika kipindi hiki.
- b) Vipindi vifupi vya mvua za nje ya msimu vinatarajiwa kuendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo, hususani katika ukanda wa ziwa Victoria pamoja na pwani ya Kaskazini katika kipindi hiki.
- c) Hali ya joto la wastani kwa kipindi cha mwezi Septemba inatarajiwa katika maeneo mengi nchini.

1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA AGOSTI, 2017

Katika kipindi cha mwezi Agosti baadhi ya maeneo ya Nyanda za juu kaskazini mashariki, ukanda wa ziwa Victoria hususani maeneo ya magharibi mwa ziwa pamoja na ukanda wa Pwani ya Kaskazini yalipata mvua zilizo nje ya msimu, pia vipindi vya upepo mkali vilijitokeza katika maeneo ya mwambao wa pwani kutokana na kuimarika kwa mgandamizo mkubwa wa hewa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi.

2.0 MATAZAMIO KWA SEPTEMBER, 2017

2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Maeneo ya kati ya Kitropiki ya Bahari ya Pasifiki pamoja na eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi kwa ujumla yanatarajiwa kuwa na joto la wastani na hivyo kutoathiri sana hali ya hewa nchini. Hali ya joto la wastani Kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantic (karibu na Angola) inatarajiwa kuendelea kupunguza mvua katika maeneo ya Magharibi ya nchi pamoja na yale ya Ukanda wa Ziwa Viktoria.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA MWEZI SEPTEMBER, 2017

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Yanatarajiwa kuwa na hali ya mvua nyepesi za nje ya msimu. Hali ya joto katika ukanda huu kwa ujumla inatarajiwa kuwa za wastani.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa. Hali ya joto katika kanda hii inatarajiwa kuwa ya wastani kwa ujumla.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): Mvua chache zinatarajiwa, katika kipindi hiki. Hali ya joto katika maeneo haya inatarajiwa kuwa za wastani.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa. Hali ya joto inatarajiwa kuwa ya wastani.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa. Hali ya joto katika kanda hii inatarajiwa kuwa ya wastani.

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa na Mbeya): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa. Hali ya joto katika kanda hii inatarajiwa kuwa ya wastani.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Hali ya ukavu kwa ujumla ikiambatana na vipindi vifupi vya upepo mkali. Hali ya joto katika ukanda huu kwa ujumla inatarajiwa kuwa ya wastani.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla. Hali ya joto katika maeneo haya inatarajiwa kuwa ya wastani.

Imetolewa na; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**